

## HISTORIA FUPI YA SIKU YA USAFI DUNIANI

### A; UTANGULIZI

#### *Mhe; Mgeni rasmi,*

usafi ni suala nyeti linalomgusa kila mtu. Usafi unayagusa maisha yetu ya kila siku, mbali na kwamba ni ustaarabu lakini linachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza magonjwa ya kuambukiza na mlipuko yanayotokana na uchafu wa mazingira kama vile Magonjwa ya mfumo wa upumuaji, Kuhara damu, Minyoo, Malaria n.k. kauli mbiu ya kidunia ni **“SIKU MOJA, SAYARI MOJA , LENGU MOJA ”** na ile ya kitaifa **“FUNGUA MACHO YAKO KUTOKA KWENYE UPOFU WA TAKATAKA NA KUWA SULUHISHO SIO UCHAFUZI”**

#### *Mhe Mgeni rasmi*

Siku ya usafi Duniani (**WORLD CLENAUP DAY**) chimbuko lake ni miaka 10 iliyopita huko **ESTONIA** ambapo asilimia 4 ya watu walijitokeza pasipo shuruti ya serikali kufanya usafi wa mazingira nchi nzima kwa masaa kadhaa tu, jambo hili lileta muamko na mvuto wa kipekee kwa jamii nzima na serikali, likapata kibali sana, liliongozwa na kauli mbiu **“NCHI MOJA, SIKU MOJA”**. Jambo hili halikubaki kuwa siri kwa watu wa Estonia tu bali lilileta muamko wa kihisia na kupokelewa na jamii mbalimbali Duniani kwa kuja na msemu wa **“DUNIA, TUFANYE” (Let’s Do it! World)**, jambo likaunganisha watu kutoka pande zote za Dunia na kuamua kuwa na siku maalumu ya usafi ambayo ni tarehe **15 septemba**. Siku hii haijabaki kama siku ya kuondoa taka ngumu tu bali ni siku ya kimkakati wa kutokomeza magonjwa ya mlipuko yanayotokana na uchafu. Kwa Tanzania Maadhimisho haya yameanza kuazimishwa kwa mara ya kwanza mwaka huu 2018.

#### *Mhe Mgeni rasmi*

Ifahamike kuwa suala la usafi si suala la urithi, kuelimika, kikabila au rangi bali ni **TABIA** ambayo **mtu yeyote** anapaswa kuwa nayo kwa kujijengea mazoea au kujizoeza kuwa msafi ili kuepukana na kadhia ya uchafu na magonjwa ya kuambukiza na mlipuko yanayotokana na uchafu.

### B: UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA USAFI WILAYANI

#### *Mhe Mgeni rasmi*

Katika wilaya yetu usafi wa mazingira unatekelezwa kwa njia shirikishi yaani wananchi, watu binafsi, mashirika ya kiserikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za kibenki mfano NMB, na serikali ya wilaya ikiwa ndiyo msimamizi mkuu wa shughullu za usafi wilayani. Mifumo

miwili ya uwekaji mazingira safi (utupaji taka ngumu) ndiyo inayotumika kutokana na eneo taka zinapozalishwa hasa kwa jamii yenyewe kufanya usafi kwenye maeneo yao;

1. Mashimo ya taka kwa maeneo ya vijijini ambayo yanapaswa kuwa mita 10 toka kwenye kaya kwa kuzingatia uelekeo wa upepo
2. Vyombo vya kuhifadhi taka (wastebins, Mifuko, Mapipa au Ndoo) kwa mjini ambapo taka husafirishwa na kumwagwa dampo

### ***Mhe mgeni rasmi***

Mbali na usimamizi wa kila siku wa shughuli za usafi wa mazingira, halmashauri imeendelea kutekeleza agizo la **Mhe Rais John Pombe Magufuli** la kusimamia na kufanya usafi kila jumamosi ya mwisho wa mwezi. Aidha mwitikio wa jamii katika suala la usafi wa mazingira ni la **wastani**, hata hivyo halmashauri imeendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuwa na TABIA ya usafi kwa kuacha tabia za uchafuzi wa mazingira

## **C: CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA USAFI**

### ***Mhe Mgeni rasmi***

Katika usimamizi na utekelezaji wa shughuli za usafi zipo changamoto kadhaa zinazoathiri zoezi hili, ambazo ni;-

1. Utayari mdogo wa wanachi kubadili tabia ya uchafuzi wa mazingira
2. Uchakavu wa magari ya kusombea taka ngumu
3. Utayari mdogo na ugumu wa wananchi katika kuchangia ada ya uzoaji wa taka ngumu
4. Ushiriki wa wastani wa wananchi katika shughuli za usafi hasa siku ya jumamosi ya usafi wa mwisho wa mwezi

## **D: HITIMISHO**

### ***Mhesahimiwa Mgeni rasmi***

Mazingira safi ni maisha yetu, mazingira safi ni uhai wetu, mazingira safi ni afya yetu, mazingira safi ni uchumi wetu hivyo kila mmoja wetu ajitafakari namna anavyoweza kuwa na mchango chanya katika kuyaweka mazingira yetu katika hali ya usafi. **Ikumbukwe usafi ni ustaarabu sharti uanze na mimi**

Naomba kuwasilisha

**"FUNGUA MACHO YAKO KUTOKA KWENYE UPOFU WA TAKATAKA NA KUWA SULUHISHO SIO UCHAFUZI"**